



Utangulizi

Katika kipindi cha Agano la Kale, sadaka ilihusu kuchinjwa kwa mnyama asiye na hatia kwaajili ya hatia ya mtu ambaye kwaajili yake mnyama huyo anachinjwa. Pale ambapo tendo la kuchinja (kwa kufuata utaratibu ulioelekezwa katika sheria) liliambatana na toba ya kweli na imani, Mungu aliitazama ile damu iliyomwagika, ikiwa ni matarajio ya msalaba wa Kristo na upatikanaji wa upatanisho.

Tunapoendelea kufikiri juu ya sadaka ya mnyama asiye na hatia, tunapaswa kukumbuka gharama kubwa ya dhambi, na tushukuru ya kwamba, ile haja ya kutoa sadaka katika hali ya mwili ilifutwa moja kwa moja (hakika moja kwa moja) kwa sadaka ya Bwana Yesu pale msalabani.

Agano la Kale

Sadaka kama ilivyoamuriwa na Mungu katika Agano la Kale

Ilikuwa ni kivuli ambacho kifo cha Kristo kulikuja kukamilisha. Lakini sadaka ya Kaini ambayo haikuwa imeidhinishwa, na ambayo Mungu alikataa, ilikuwa ni maandalizi ya karibu sadaka zote za wanadamu na ibada za sanamu na ukosefu wa maadili.

Mwanzo **4:3, 5; 8:20; 22, 13; 31:54; 46:1**; Kutoka **18:12; 12:3-13**;

Mambo ya Walawi **1:2-4**; sura ya 16; Kumbukumbu **32:16-17**; 1 Samueli **15:22**;

Mithali **17:1**; Waebrania **11:4; 10:1**; 1 Wakorintho **10:20**

Chini ya sheria mambo mawili yalikuwa ni ya muhimu katika upatanisho:

1. Imani – katika utoaji wa sadaka ya damu.
2. Toba – Isaya **1:13, 16, 18**; Hesabu **5:7** (toba na pale ilipowezekana ukombozi)

Sehemu muhimu ya utaratibu wa utoaji wa sadaka ilikuwa ni kufuata utaratibu wa kujikosha. Utaratibu huu ulionyesha umuhimu wa kujisafisha dhidi ya unajisi unaoletwa na dhambi. Hii ilikuwa ni maandalizi ya ubatizo wa Kikristo ambao ni ishara ya utakaso dhidi ya dhambi. Tazama kwa mfano, Mambo ya Walawi **14:8-9**; Hesabu **8:7; 19:13**; pia Matendo **22:16**.

Katika Agano Jipya

Mwana kondoo alikuwa ni kielelezo cha muhimu aliyetumika kama mnyama wa sadaka. Tazama kwa mfano, Mwanzo **22:13**, mwana kondoo ambaye hatimaye Mungu angemtoa alikuwa ni Bwana Yesu. Agano Jipya linaanza na kilio cha ushindi cha Yohana Mbatizaji akisema, 'Tazama Mwana kondoo wa Mungu (Yohana **1:36**). Bibilia takatifu anaishia na kitabu cha Ufunuo, ikionyesha maono ya utukufu wa Mwana Kondoo aliyechinjwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu (Ufunuo **13:8**)

Yohana **1:36; 3:16**, 1 Wakorintho **5:7**; Waebrania **9:13-14**; Ufunuo **13:8**

Kumbuka: Kuna hoja muhimu inayosema kwamba Mwana Kondoo wa Mungu, anapaswa kutafsiriwa kwa uhakika zaidi kuwa ni 'Kondoo (dume) wa Mungu'. Huyu kondoo (dume) ambaye angechinjwa alipaswa kuwa ni kondoo ambaye amepevuka, ambaye amefikia kilele cha kukua kwake, ambaye maisha yake yamekuwa ya muhimu. Liliikuwa ni jambo la thamani sana kwa mmiliki wa yule kondoo na ilihusu gharama halisi kwake katika kumtoa yule kondoo kama sadaka. Pia kimvuli cha Kristo kinaonekana katika kitabu cha Mwanzo **22:13**– na hapa mnyama ambaye alipaswa kutolewa kama sadaka anatajwa

kuwa ni kondoo (dume). Bwana Yesu, alipotolewa kama sadaka pale msalabani kwaajili ya dhambi zetu, alikuwa amefikia kilele cha maisha yake [umri unaokisiwa ni kama miaka thelathini na tatu hivi], akiwa ameishi kwa uhakika bila ya kutenda dhambi).

Sadaka ya Kristo kwaajili ya dhambi ya ulimwengu ilikuwa ni kitendo cha mwisho

Hakuna njia nyingine, wala injili nyingine ya kweli. Pazia katika hekalu la Yerusalemu lilichanika kutoka juu mpaka chini, ishara ya wazi kwamba njia ya kwenda kwa Mungu sasa iko wazi kwa kila mtu. Hakika, kabla Wakristo hawajajulikana kama ni 'Wakristo', walijulikana kama ni watu wa 'Njia'. Tangu mwanzo kabisa wa kanisa, Wakristo walizingatia kuwa utoaji wa wanyama au uvumba haukuwa na ufanisi. Walikubali tu utoaji wa 'sadaka' za maombi, za sifa na shukrani, wakiwa katika moyo wa kweli, wa unyenyekevu na uliopondeka, kwamba hili ndilo lilikuwa tendo la shukrani linalo kubalika mbele ya Mungu wa haki, anayekomboa. Kwakuwa sasa hakuna tena sadaka za upatanisho, kinachofuatia ni kwamba hakuna tena ukuhani (wa aina hii). Kwa hali yoyote ile, hekalu la Wayahudi lilikuwa livunjwe katika muda si mrefu (ifikapo mwaka 70BK) na ule ukuhani wa kale usiwepo tena. Baadala yake Mungu ameunda miongoni mwa wale walio na imani ya kweli juu ya Bwana Yesu ukuhani wa kifalme – ukuhani wa wote waaminio (1 Petro 2:9).

Yohana 10:18; 12:32-33; 17:4; 19:30; Warumi 3:25; 5:9; 1 Wakorintho 6:20; 2 Wakorintho 5:19; Wagalatia 3:13; Waefeso 1:7; Wakolosai 1:21-22; Waebrania 9:12; 10:10-18; 1 Petro 1:18-19; 2:24

Mambo mawali ni muhimu kwaajili ya upatanisho chini ya neema

1. **Imani katika toleo la damu ya Yesu** (tazama Warumi 3:24-25; Waebrania 10:12).
2. **Toba** hali ya kiufahamu ya kugeukia mbali (kuachana) na dhambi na kufanya uamuzi wa kuishi maisha yanayokubalika na Mungu. Kiuhalisia, ni hali ya kubadilika kiakili, si tu katika mipango ya binafsi, malengo na imani, lakini ni mabadiliko ya kiutu ambayo hadi sasa utu huo unamuelekeo wa dhambi, lakini baadaye utaelekea kwa Mungu (Matendo 20:21). Toba hii si kitendo kinachojisimamia peke yake, bali nidhamu ya kiakili, inayotia moyo mabadiliko ya tabia na kuhusisha pale inapobidi, matendo yanayoleta faida katika maisha (Tazama Luka 19:8).

Ubatizo wa Kikristo ni ishara ya kutakaswa kwa moyo dhidi ya dhambi

Tazama tena maelezo juu ya utaratibu wa kuosha katika Agano la Kale

1 Petro 3:20-21 [Pia tazama sura ya 31 juu ya ubatizo]

Kutokana na Kanisa la Kikatoliki la Rumi, sakramenti ya toba inahusu masuala ya kupondeka, kutubu, na kuridhika. Ndipo kuhani anapotiwa nguvu kutangaza msamaha. Hata hivyo, katika Agano Jipya, hakuna mahusiano kati ya 'mfumo wa kisakramenti' na kutangaza kwa msamaha kwa kuhani ambaye ni mwanadamu. Hakika, wazo hili linaendeanza na hitaji la mwenye dhambi yeye binafsi kumgeukia Mungu katika toba, na kupokea msamaha kupitia Kristo ambaye peke yake ndiye mpatanishi (1 Timotheo 2:5) ambaye ndiye Kuhani Mkuu wa watu wake.

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK
www.sovereignworldtrust.org.uk

Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.
Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - www.christian-publications-int.com
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron- Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4